> *2Wakorintho 13:14 "Neema ya Bwana Yesu Kristo, na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nanyi nyote".*

---

Hii ni salamu ya kumalizia ambayo mtume Paulo aliwaandikia wakorintho, na watu wote watakaousoma waraka huo (ikiwemo mimi na wewe).

Maneno haya, yamegusa Nyanja zote tatu za Kusudi la Mungu kwetu sisi wanadamu.

> Paulo anaanza kwa kusema, Neema ya Bwana Yesu Kristo, ikae nasi; Akiwa na maana kuwa mpaka sisi tukamilike, mpaka sisi tushinde, tunaihitaji hii neema ya Yesu Kristo wakati wote itembee na sisi, tukipungukiwa neema, basi ni ngumu kuweza kuushinda ulimwengu. Na neema hii inaanza kutembea juu ya mtu kwa mara ya kwanza pale anapookoka.

> Anasema tena, Pendo la Mungu likae nasi: Ni kwa njia ya upendo Mungu alitukuomboa (Yohana 3:16). Hivyo na sisi tukiukosa Upendo, haijalishi tutakuwa washirika wazuri kiasi gani, haijalishi tutafanya miujiza mingi kiasi gani, tutanena kwa lugha za malaika nyingi kiasi gani, bado sisi tutabakia kuwa si kitu. Hivyo Pendo la Mungu linapokaa ndani yetu basi Mungu

anakuwa karibu na sisi. Na pendo la Mungu ndio lile linalozungumziwa katika *1Wakorintho 11:1-8*

Na ndio huo Paulo alikuwa analiombea kanisa ukae ndani yao.

> Anamalizia na kusema pia Ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nanyi nyote; Hii ikiwa na maana palipo na Roho Mtakatifu pana ushirika.. Sisi kama wakristo tuliookoka ni jukumu letu kuutunza ushirika wa Roho tukinia mamoja, tukiifanya kazi ya Mungu..

> *Waefeso 4:3 “na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani.*
>
> *4 Mwili mmoja, na Roho mmoja, kama na mlivyoitwa katika tumaini moja la wito wenu.*
>
> *5 Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja.*
>
> *6 Mungu mmoja, naye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote na katika yote na ndani ya yote”.*

Mambo haya matatu yakienda pamoja na sisi, basi Mungu naye ataenda pamoja na sisi, lakini tukipungukiwa kimoja wapo, aidha neema, au Upendo, au Ushirika, ni ngumu kusimama kama Kanisa.

Hivyo mimi na wewe tujitathmini ni wapi, hatujakamilisha, kisha tukamilishe, Na Bwana atusaidie.

Shalom.

Tafadhali washirikishe na wengine habari hizi njema, na pia kama utapenda tuwe tunakutumia mafundisho ya Neno la Mungu ya mara kwa mara kwa njia ya email yako au Whatsapp basi tutumie ujumbe kwenye namba hii +255 789001312

Mada Nyinginezo:

> *UNYAKUO.[1]*

> *KWANINI MUNGU ALIMTUMIA MUSA KWA VIWANGO VILE?[2]*

> *UPONYAJI WA ASILI[3]*

> *JE UDHAIFU WANGU UNAWEZA KUZUIA INJILI?[4]*

> *ADAM NA EVA.[5]*

> *Amin, nawaambia, Kizazi hiki hakitapita..[6]*

Rudi Nyumbani:[7]

Share on:
WhatsApp
Endnotes:

1. UNYAKUO.: https://wingulamashahidi.org/2018/07/19/unyakuo/
2. KWANINI MUNGU ALIMTUMIA MUSA KWA VIWANGO VILE?: https://wingulamashahidi.org/2020/01/25/kwanini-mungu-alimtumia-musa-kwa-viwango-vile/
3. UPONYAJI WA ASILI: https://wingulamashahidi.org/2020/08/07/uponyaji-wa-asili/

4. JE UDHAIFU WANGU UNAWEZA KUZUIA INJILI?: https://wingulamashahidi.org/2020/08/19/je-udhaifu-wangu-unaweza-kuzuia-injili/
5. ADAM NA EVA.: https://wingulamashahidi.org/2020/07/19/adam-na-eva/
6. Amin, nawaambia, Kizazi hiki hakitapita..: https://wingulamashahidi.org/2018/07/17/amin-nawaambia-kizazi-hiki-hakitapita-hata-hayo-yote-yatakapotimia/
7. Rudi Nyumbani:: https://wingulamashahidi.org